Inaendelea pale ilipoishia mwaka wa fedha 2020/2021, tulitegemea baada ya kuanza kutumia mpango mpya katika Utumishi (New Scheme of Service) mambo yangekuwa bora kwa walengwa (Watumishi) kama ilivyotegemewa kuwa, huwezi amini mambo yamekuwa tofauti. Hadi naandika taarifa hii ndiyo mwaka wa fedha unaanza 2023/2024.

Habari za ndaaaani zinasema Wakala (BRELA) kabla ya mwaka huo tajwa hapo juu ilikuwa inatumia mfumo wa rasilimali watu ambao wenye dhamana ya Utumishi wa Umma (OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma) ilikuwa haiutambui; jitihada zilifanywa hapo awali hadi kufikia mwaka huo mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma akaridhia na kubariki mfumo mpya yaani *scheme of service* mpya iliyoanza kutumika mwaka 2020/2021.

Madhara ya huu mfumo mpya yamekuwa na athari zifuatazo hasa kwa wale waliokuwepo kwenye taasisi hiyo hapo awali kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo mpya; na madhara hayo yako hivi: -

(i) Waajiriwa wa awali yaani kuanzia 2019 kurudi nyuma bila kujali ana miaka mingapi kwenye Utumishi wa Umma, uzoefu na elimu aliyo nayo hadi wakati huo, wote walitambuliwa sawa na wale walioajiriwa kuanzia mwaka 2020 kwa maana ya vyeo, mishahara na maslahi mengineyo;

(ii) Waajiriwa wa zamani na wapya wanapoenda popote kikazi wanapojitambulisha, wote wanaonekana ni wapya na wamejiariwa mwaka 2020 na kuendelea;

(iii) Ajabu iliyopo, mfumo huo hauna madhara hasi kwa Watumishi wa kuhamia kutoka sehemu nyingine katika Utumishi wa umma na wale ambao ni waajiriwa wapya (mwaka 2020 na kuendelea) katika Utumishi wa Umma.

Ukitizama kwa haraka haraka mfumo mpya umekuwa ni adhabu kwa Watumishi wa zamani na thubutu kusema hii ni *psychological torture*.

Maswali ninayojiuliza hadi hivi sasa, na ambayo sijapata majibu yake rasmi hadi hivi sasa ni haya: -

(a) Inawezekanaje Mtumishi akaadhibiwa kwa uzembe/makosa uliofanywa/yaliyofanywa na mwaajiri wakati ikiwa yeye hajachangia chochote kwa uzembe/makosa huo/hayo?

(b) Kwanini mwaajiri hakuhakikisha kuanza kuwapanga Watumishi wa zamani wakiwa kwenye nafasi wanazostahili kwa kuzingatia umri wa kila mmoja katika Utumishi wa Umma bila kusahau kiwango cha elimu alichokuwa nacho kwa wakati huo wa mabadiliko yaliyotokea; halafu ndiyo wafatie hao wengine?

(c) Najua kuna sheria na kanuni zinazosimamia Utumishi wa Umma, ina maana sheria ilivyo sasa haina sehemu yeyeto inayotoa ruhusa kwa hawa wa zamani wakakaa sehemu ambayo kila mmoja anastahili kuwepo (cheo) kwa kuzingatia umri aliyo tumikia Utumishi wa Umma bila kusahau elimu aliyo nayo kwa wakati huo?

Inavyofahamika kwenye sheria *wherever there is a general rule there is an exception to that general rule*; hii maana yake nini, endapo hakuna kifungu kinacho sema kuhusu hawa wa zamani dhidi ya mabadiliko ya kimfumo wa utumishi kwenye taasisi husika

(BRELA) nilitegemea Mkuu wa Idara ya Utawala na rasilimali watu apeleke ombi Utumishi (mwenye sheria yake) kuwa kuna hawa watu tunaomba haki itendeke dhidi yao kutokana na mabadiliko yaliyofanyika ndani ya taasisi.

Kwasababu, inavyoaminika hadi sasa hakuna kinachoshindika kwa binadamu isipokuwa kufufua kiumbe hai ambaye tayari amekwisha kufa. Idara husika kama ingekuwa na nia nzuri kwa wateja wake (Watumishi); ni Imani yangu haya yasingejitokeza.

Katika hili hata Rais-URT katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani 2023 katika hotuba yake alisema anajua kuna watu wengi kwa muda mrefu hawajapandishwa madaraja na akatoa ruhusa ya Watumishi wapandishwe kwa msereresko.

Pamoja na mambo mengine, Idara ya Utawala na rasilimali watu imezingua kwenye maeneo yafuatayo: -

I. Kuuaminisha umma kuwa hadi sasa Watumishi waliojiriwa na taasisi hapo zamani na waliojiriwa kuanzia 2020 tuwatambue kuwa wote wameajiriwa mwaka mmoja 2020;

II. Kuuaminisha umma hadi sasa Watumishi wa kuhamia ndiyo waajiriwa wa zamani ndani ya taasisi hiyo;

III. Taswira iliyotengenezwa hadi hivi sasa, ni pale Mtumishi wa zamani anapojitambulisha kwa cheo chake, anaonekana ni mwaajiriwa mpya katika taasisi na Utumishi wa Umma kwa ujumla wake.

Nilitegemea Idara husika kwa kushirikia na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma wengepambana kuhakikisha kuwa tofauti hizo zisijitokeze; kwa asili, huwezi kuwaaminisha watu kuwa wazazi na watoto kuwa wote wako sawa.

Kama hiyo haitoshi, inawezekanaje taasisi ya umma haina mpango wa kusomesha watumishi wake; yaani mtumishi anajisomesha kuanzia stashahada, shahada ya kwanza na wengine hadi shahada ya pili na mwaajiri ametulia tu wala hajigusi kwa lolote kuhusu elimu ya Mtumishi wake. Yaani ni aibu mbayo na uhakika hata sheria husika hailikubali hili.

Jingine, unakuja na uamuzi wa Watumishi kuvaa sare; ambalo siyo jambo baya. Ubaya katika hili, ni taasisi husika kulisimamia hili bila ya kutoa fedha za sare au sare stahiki kwa Watumishi wake; kwa maana nyingine, Watumishi wanajitegemea sare hizo kwa fedha binafsi ambapo maamuzi hayo yalifanywa na mwaajiri bila hata ya kuwashirikisha Watumishi katika kujadili kuhusu suala hilo.

Sasa ndiyo nimeanza kumuelewa yule jamaa wa OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma aliposema “kuna maamuzi ya kijinga huwa yanafanywa huko chini huwezi amini kama ndiyo mtu wa utawala kafanya maamuzi husika.”

Kimsingi, rasilimali watu ndiyo rasilimali kubwa kuliko rasimali nyingine yeyote katika taasisi yeyote duniani; ndiyo maana katika nchi zilizoendelea rasimali hii inaangaliwa kwa umakini sana. Sikutegemea moja ya taasisi muhimu hapa nchini inawezaje kufanya makosa ya kiwango hicho kwa Watumishi hawa wa Umma na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma (wenye sheria yao) wapo kazini.

Hii ni taasisi muhimu sana kwenye eneo la biashara na uwekezaji hapa nchini, kwa mantiki hiyo Idara ya Utawala na rasilimali watu ndani ya taasisi inatakiwa iwe inafanya kazi kiweledi na kuzingatia sheria zilizopo lakini pia busara na nidhamu ya hali ya juu sana katika kuwa hudumia Wateja wake (Watumishi); nashangaa kuona makosa yote hayo anafanyiwa mteja na bado wahusika wa Idara hiyo wapo. Kwa kifupi, hatutegemei mteja aanze kudai haki yake wakati wahusika wapo kwaajili ya kuhakikisha kila kitu kuhusu Mtumishi kinakwenda sawa na anapewa mrejesho kwenye kila jambo linalohusu ajira yake kwa mfano kupenda cheo, mshahara, nyongeza ya mshahara na mengineyo yanayofanana na hayo kwa Mtumishi (Mteja).

Uchunguzi uliofanyika kwa muda mrefu hadi sasa umebaini hayo ambayo yana madhara ya moja kwa moja kwa Watumishi (Wateja); mimi pamoja na timu yangu tutaendelea kuangazia yale yenye athari hasi kwa Watumishi kwa kadri yanavyoibuka katika taasisi hii (BRELA) ambayo yatakuwa yameibuka mpaka tutakapoona taasisi husika inajali rasilimali watu kwa kiwango cha kitaifa na hata kimataifa pia.

Naamini OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara husika wapo kazini na watayafanyia kazi hayo tuliyo yaona hadi hivi sasa kuwa hayako sawa kwa Watumishi waliopo katika taasisi tajwa tangu mwaka 2020.

Wanajamvi humu ndani tunawasilisha kwenu ili mjionee ni kwa jinsi gani mambo yanavyo endeshwa katika taasisi hii ya umma ambayo niliamini ina utaratibu mzuri wa kuajiri na kuwajali Wafanyakazi wake; ndiyo maana wahenga walisema, “umdhaniaye ndiye kumbe siye.” Jamani! Hii ina tofauti gani na kampuni iliyo changamka ya wale jamaa zetu wenye asili ya Asia?

Wanajamii, OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Viwanda na Biashara kazi iendelee.